# ‘Iktibasi’ katika Tenzi za *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi*

*Beja, S. Karisa*
na
*Abdulrahman Mwinyifaki*

**Ikisiri**

Makala haya yanatazama tenzi za kale za Kiswahili kwa mkabala wa kitabu kitukufu cha Kurani na Sunnah za Mtume Muhammad (SAW). Wahakiki wengi wamechambua tenzi hizi za kale na kutoa maoni kwamba zina maudhui ya dini ya Kiislamu. Hata hivyo ushahidi halisi wa jinsi watunzi walivyochota maudhui yao kutoka kwenye Kurani Tukufu na Sunnah[1] haujawekwa bayana na utafiti wowote. Makala haya yamelenga kuziba mwanya huu kwa kuonesha jinsi watunzi wa tenzi za *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi* walivyochota kutoka kwenye Kurani Tukufu na Sunnah kifungu baada ya kifungu na kujenga maudhui yao ya dini ya Kiislamu katika fasihi bila wao kusema kazi zao zinatokana na Kurani Tukufu na Sunnah. Mfumo huu wa kutumia Kurani Tukufu na Sunnah bila kubainisha kuwa ni Kurani Tukufu au Sunnah kwa lugha ya Kiarabu huitwa “Iktibasi”. Makala haya yameongozwa na nadharia ya Uislamu. Taib (2004) ameeleza kwa kirefu nadharia hii kwamba imejikita katika nguzo tano za Uislamu. Lengo kuu ni kuonyesha jinsi watunzi wanavyoweza kuhuisha vifungu vya Kurani Tukufu na Sunnah katika miktadha halisi kwa njia ya kubuni na kuvitumia kama misingi ya mahubiri ya mtu binafsi na kwa umma. Katika makala haya tunaona kwa yakini uhusiano uliopo kati ya dini ya Kiislamu na fasihi. Dini inanufaishwa na fasihi kupitia mahubiri yenye msingi wa kifasihi nayo fasihi inasambazwa kupitia mahubiri ya kidini. Mbali na kudhihirisha uhusiano wa dini na fasihi makala haya ya uchanganuzi wa tenzi hizi ni muhimu kwa maulamaa na waandishi wa fasihi kwa kuona jinsi wanavyoweza kuchota vifungu teule vya Kurani Tukufu na Sunnah kama msingi wa mahubiri kwa wanajamii kwa njia za kifasihi.

## 1.0 Utangulizi

Tenzi ni utanzu wa ushairi wa Waswahili ambao ni mkongwe. Hata hivyo, kiasi cha utunzi wake kwa sasa kimepungua. Zamani tenzi zilikuwa zikitungwa kwa wingi lakini siku hizi hazitungwi kwa wingi ukilinganisha na utunzi wa mashairi. Hili ni suala ambalo linahitaji kutafitiwa ili utunzi wa tenzi uendelezwe kama

---

[1] Sunnah haitoki moja kwa moja katika Kurani; inatokana (i) Failiyyu - matendo aliyofanya Mtume Mohammad (S.A.W), (ii) Qauliyyu - maneno aliyosema Mtume Muhammad (S.A.W) kwa wafuasi wake na (iii) Takririyyu – kimya alichotumia Mtume Muhammad (S.A.W) kuashiria kukubalika kwa jambo ambapo kama jambo halikuwa zuri Mtume angalisema kuwa si zuri.

zamani, au sivyo tutabaki kuhakiki tenzi hizi hizi za kale. Tenzi za kimapokeo ni tungo ambazo kimuundo zimepangwa mafungu katika beti ndogo zenye mishororo isiyozidi minne na idadi ya mizani isiyozidi kumi na moja. Tenzi pia zina sifa ya kuwa na beti nyingi. Kwa mfano, *Utenzi wa Hamziya* una beti zaidi ya elfu moja. Kawaida tenzi huwa na vina. Beti za tenzi mara nyingi huwa hazijitoshelezi kinyume na beti za mashairi. Vilevile watunzi wa tenzi huwa na jadi ya kutaja majina yao na pia kutaja tarehe ya kuzaliwa kama njia ya kutia muhuri tungo zao. Tenzi za kale pia zilikuwa na sifa ya kuanza kwa jina la Mwenyezi Mungu na kutaja jina la Mtume Muhammad (S.A.W) na swahaba zake wanne, Kwa mfano utenzi wa *Al-Inkishafi*. Hizi ni sifa ambazo ziliingia katika tenzi kulingana na ufundi na mazoea ya watunzi wa tenzi za Kiswahili. Kimaudhui tenzi zinaweza kubeba maudhui yoyote ila tu tenzi za kale zilitumiwa kuelezea maudhui ya kidini. Nyingi ya tenzi za awali za Waswahili zilikuwa ni tafsiri ya tenzi za Uarabuni kama vile *Utenzi wa Hamziya* na *Utenzi wa Chuo cha Tambuka*. Tenzi za Uarabuni zilikuwa zinazungumzia maudhui ya dini ya Kiislamu ndio maana tenzi za awali za Waswahili nazo zikawa zinatungwa kuelezea maudhui ya dini ya Kiislamu.

.

## 2.0 Lengo la Makala

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu tenzi za Kiswahili hasa tenzi za *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi*. Wachanganuzi wengi wamesema kuwa tenzi hizi zimesheheni maudhui ya dini ya Kiislamu (Hichens, 1972; Shahid, 1980 na Mulokozi, 1991). Hata hivyo dai hili halijawekwa bayana na utafiti wowote hasa kwa kuonesha jinsi watunzi wa tenzi hizi walivyochota vifungu teule vya Kurani Tukufu na Sunnah na kuvihuisha kifasihi na kuumba tenzi hizo kama 'iktibasi'. Makala haya yananuia kuziba pengo hili la kitaaluma na kiutafiti kuhusu uchanganuzi wa tenzi hizi za kale kama mfano wa mfumo wa 'iktibasi'.

## 3.0 Misingi ya Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Kiislamu (Taib, 2004) katika fasihi, ambayo mihimili yake kwanza, fasihi lazima iendeleze Uislamu ambao nguzo-mama yake ni kukiri kwamba kuna Mungu mmoja naye ni Allah na Muhammad ni Mtume wake kama inavyokaririwa katika kitabu kitakatifu cha Kurani. Pili, fasihi ilenge kukosoa makosa ya binadamu kwa misingi ya mafundisho ya dini ya Kiislamu ambayo yanachukua Kurani Tukufu na Sunnah kama mwongozo wa maisha kamili ya mwanadamu. Kwa misingi hii, Waislamu wanashauriwa waswali mara tano kwa siku, watoe zaka, wafunge mwezi mtukufu wa Ramadhan na wahiji mara moja wanapopata nafasi ya kufanya hivyo. Tatu, kwamba Mwenyezi Mungu (S.W.T) ni mwenye rehema na yeyote anayetubu makosa yake atamsamehe.

Kwa msingi wa mhimili wa kwanza, makala haya yanaonesha jinsi watunzi wa tenzi za kale za *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi* walivyochota moja kwa moja vifungu mahususi kutoka Kurani Tukufu na Sunnah. Vifungu hivyo vilihusishwa na miktadha halisi ya maisha ya jamii kwa njia ya ubunifu kama namna moja ya kutumia fasihi kueneza dini ya Kiislamu miongoni mwa Waswahili ambao wengi wao nyakati hizo walikuwa wakitumia fasihi simulizi kufundisha maadili kwa vijana na watu wazima kwa jumla. Kwa msingi wa mihimili ya pili na wa tatu wa nadharia ya Uislamu tutaona jinsi fasihi inavyoweza kuwa chombo mwafaka cha kuhubiria mafundisho ya dini ya Kiislamu kwa watu binafsi na jamii kwa jumla, kwani tenzi hizi zilitungwa kwa lengo la hadhira pana zaidi. Hivyo, mbinu ya kutumia tenzi wakati huo ilisaidia kuwajulisha Waswahili mafundisho ya Uislamu na kuishawishi jamii ya Waswahili kujiunga na dini ya Kiislamu kwa sababu wengi walikuwa hawajui kusoma Kurani Tukufu. Yaliyomo katika Kurani Tukufu na Sunnah yaliwasilishwa kwa waumini na waumini tarajiwa kupitia tenzi. Makala haya yanamulika mienendo inayotarajiwa kwa Waislamu kulingana na Kurani Tukufu na Sunnah kupitia 'iktibasi' ya tenzi za kale.

## 4.0 Msingi wa Kihistoria

Makala haya yanahusu ufafanuzi wa tenzi za kale kama tungo zinazotokana na Kurani Tukufu na Sunnah na kutumika kama nyenzo za mahubiri ya Uislamu kupitia fasihi. Ili kuelewa vizuri suala hili la tenzi na Uislamu itabidi turejelee nyuma katika kipindi cha chimbuko la Ushairi wa Kiarabu (Kasida). Hii ni kwa sababu utenzi wa Kiswahili ulipata athari kubwa kutoka kwa ushairi wa Kasida kimuundo na kimaudhui. Kwa hakika, ushairi wa Kiswahili kwa jumla una historia ndefu, na inaaminika kuwa chimbuko lake ni fasihi simulizi ya Waswahili kwa hivyo ushairi wa Kiswahili ni mkongwe, ndipo mara nyingi huitwa ''Ushairi jadi''. Ushairi jadi wa Kiswahili uliendelezwa katika utanzu wa tenzi kuliko mashairi kwa sababu tenzi na nyimbo zilizoeleka zaidi kuliko mashairi ambayo yaliingizwa juzi juzi baada ya kuletwa maandishi. Ushairi katika jamii nyingi za Kiafrika, Waswahili wakiwemo, ulianza kama fasihi simulizi kupitia kipera cha nyimbo.

## 4.1 Ushairi wa Kasida Uarabuni

Kulingana na ushahidi wa kihistoria, tenzi za Kiswahili ziliathiriwa sana na ushairi wa Uarabuni ulioitwa Kasida, ambao ulichimbuka Uarabuni mnamo miaka ya 500 BK (Shahid, 1980). Hiki ni kipindi cha kabla ya majilio ya Uislamu. Kasida nyakati hizo ulikuwa ni ushairi ambao ulihusu maudhui mengi na yenye malengo tofauti tofauti kuhusiana na mazingira ya jangwani, kama alivyoyaona mtunzi, na kuyaeleza kwa kirefu. Msanii aliyejulikana zaidi nyakati za chimbuko la Kasida ni Imrul-Qays (Shahid, 1980). Kasida zake zilikuwa zina mvuto wa mdundo uliovyazwa na urari wa vina na msamiati teule ulioeleza

mazingira ya jangwani. Kufikia karne ya sita (550 BK), ushairi wa Kasida ulianza kutumika kama wasifu na ukaendelezwa hadi majilio ya Uislamu.

## 4.2 Kasida na Majilio ya Uislamu

Uislamu ulipoletwa na Mtume Muhammad (S.A.W) ulikuta ushairi upo. Nyakati hizo kulikuwako washairi mashuhuri katika kabila la Kiarabu kama vile Immil Qais, Zuheer bin Khaab, Hassan bin Thabit na Farazdak. Kwa umahiri wao katika utunzi Mtume Muhammad (S.A.W) aliwatumia washairi hawa kuwahamasisha wanajeshi wake wakati wakienda katika vita vya jihad. Hususan, washairi Hassan bin Thabit na Zuheer bin Khaab waliwahi kutuzwa vishali kwa umahiri wa utunzi wao (Bohar Muslim, 2005). Ni kwa njia hii ambapo Uislamu uliingizwa katika Kasida. Kutokana na maelezo haya inabainika kwamba ushairi ulianza kutumika kitambo kama chombo cha dini ya Kiislamu, hususan katika kuwahamasisha Waislamu kuhusu Uislamu. Kuingizwa kwa Uislamu katika Kasida kulionekana zaidi, kwanza, katika matumizi mengi ya istilahi na mawazo ya Uislamu na pili, katika utumiaji mwingi wa maelezo ya hisia za kidini katika tungo zilizotungwa hasa katika kipindi cha uongozi wa Umayyad (Shahid, 1980). Ushairi wa Kasida ulianza kuelezea maudhui ya aina tatu. Kwanza, Kasida ilitumika kuelezea mafundisho ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu (S.W.T) kwa mwanadamu kuhusu kiyama kwa wasioamini kama inavyodhihirika katika Kurani Tukufu na Sunnah. Pili, Kasida, ilitumika kuelezea na kuhamasisha waumini juu ya Vita vya Jihad na dhana ya kuhiji. Tatu, Kasida ilitumika kuelezea sifa na safari ya uhamiaji wa Mtume Muhammad (S.A.W) kutoka Makka hadi Madina. Kwa hivyo, tunaona kwamba ushairi wa Kasida ulipoletwa katika jamii ya Waswahili ulikuwa tayari una majukumu ya kuhamasisha watu juu ya Uislamu. Hii ndiyo sababu iliyowafanya watunzi wa tenzi za Kiswahili kutumia tenzi zao kuhubiria mafunzo ya Uislamu kwa mfumo wa 'iktibasi'.

## 4.3 Tenzi na Majilio ya Waarabu Afrika ya Mashariki

Baada ya kifo cha Mtume Muhammad (S.A.W) kulibuniwa huko Uarabuni mfumo wa Ukhalifa uliomchagua kiongozi wa kidini atakayechukua mahali pa Mtume Muhammad (S.A.W). Mfumo wa Ukhalifa ni utaratibu ulioanzishwa na wazee wa Kiislamu wa kumteua kiongozi wa Waislamu baada ya kufa Mtume Muhammad (S.A.W). Utaratibu huu ulitekelezwa na jopo la wazee na aliyeteuliwa aliitwa 'Califah Rasul Allah' yaani mchukua mahali pa Mtume wa Mungu. Katika mfumo huu, Makhalifa waliochaguliwa mwanzo kwa kufuatana ni Abu Bakar, Umar, Uthman na Ali. Makhalifa hawa waliufuata vizuri mfumo huu wa Ukhalifa lakini Makhalifa waliofuata waliuharibu mfumo huu. Katika kipindi cha Ukhalifa wa ukoo wa Umayyad (661-750), Khalifa Muawiyah aliufanya mfumo huu kuwa jambo la ukoo na akamchagua mtoto wake Yazid

kuanza mfumo wa Ukhalifa kwa misingi ya ukoo. Yazid aliendeleza Ukhalifa wa ukoo ambao ulikithiri kwa Makhalifa 14 waliofuata, mpaka wakati ukoo wa Umayyad ulipopinduliwa na ukoo wa Abbasid (Shahid, 1980). Baada ya mapinduzi haya Abu Abass, aliyejulikana kwa lakabu 'Muuaji' alifanya Ukhalifa kuwa jambo la ufalme katika ukoo wa Abbasid. Ukhalifa wa kifalme uliendelezwa na Makhalifa 10 baada ya Khalifa Abu Abbas, mpaka mwaka 1250 ambapo kulizuka Vita vya Ukhalifa miongoni mwa koo nyingi zilizopinga au kuwania Ukhalifa. Ni wakati wa vita hivi vya Ukhalifa ambapo koo nyingi za Waarabu zilizotorokea Afrika Mashariki na kuishi huko kabisa. Baadhi ya koo hizo ni Maawiya waliohamia Lamu, Nabhanny waliohamia Pate na ukoo wa Sayyid kutoka Hadhrami waliohamia visiwa vya kusini kama vile Zanzibar (Salim, 1973). Uhamiaji kwa wingi wa koo za Waarabu ambao walikuwa ni Waislamu ulileta athari kubwa katika taratibu za maisha na utamaduni wa Waswahili (Salim, 1973). Kwanza, Waarabu hawa walileta dini ya Kiislamu. Pili, walileta ushairi wa Kasida ambao ulikuwa unatumiwa kuelezea maudhui ya dini ya Kiislamu huko Uarabuni. Kasida walizoleta zilitafsiriwa kwa Kiswahili na kuandikwa kwa hati za Kiarabu. Tafsiri za Kasida ziliingia katika fasihi ya Waswahili kama tenzi / tendi. Baadhi ya Kasida zilizotafsiriwa kama tenzi ni Kasida "Umma-ul-Qura" ambao ulitafsiriwa na Sayyid Aidarus mwaka 1749, na ukajulikana kama *Utenzi wa Hamziya*. Utenzi huu pia uliitwa kwa Kiarabu "Kasidatu'l Hamziya Fi'I Mada'hi 'n Nabawiya" (Kasida ya kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) inayoishia na herufi ya hamza. Utenzi huu ulitafsiriwa kutokana na Kasida ya awali iliyokuwa imetungwa na Sharafu'd-din Abu Abdalla Bin Mohammad bin Said-Dilasi al-Busiri al- Sanhaji (1213-1302) wa Moroko, ambaye katika ujana wake alisoma dini ya Kiislamu katika mji wa Cairo (Shahid, 1980).

## 4.4 Tenzi katika Jamii ya Waswahili

Kutafsiriwa Kasida na kuingizwa katika fasihi ya Waswahili kama tenzi kuliimarisha utunzi wa tenzi miongoni mwa Waswahili. Hivyo tenzi nyingi zilitungwa, kwa mfano *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Fatuma*, *Utenzi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Aidha, Waarabu walipokuja walileta pia lugha na hati za Kiarabu. Hati za Kiarabu zilifanya tungo za Kiswahili, zikiwemo tenzi, zianze kuandikwa kwa Kiswahili kwa kutumia hati za Kiarabu. Katika historia ya tungo za Kiswahili *Utenzi wa Swifa ya Mwana Manga/Kumsifu Yanga* ndio utenzi ulioandikwa kwanza mwaka 1531 ukafuatiwa na *Utenzi wa Hamziya* mwaka 1652 na utenzi wa *Siri Usirari* mwaka 1663 (Mulokozi, 1999). *Utenzi wa Tambuka* na *Utenzi wa Hamziya* zilichukuliwa kama kielelezo cha kutungia tenzi zilizoandikwa baadaye, hasa kimaudhui, kwa sababu zote zilizungumzia mambo yahusianayo na dini ya Kiislamu.

## 4.5 Uislamu na Utunzi wa Tenzi

Dini ya Kiislamu ilipoletwa miongoni mwa Waswahili ni dhahiri shahiri kuwa, ilipokelewa kwa mikono miwili. Baada ya kupokea Uislamu Waswahili walifundishwa maadili ya Kiislamu na kusoma Kurani Tukufu katika madrasa. Waswahili waliohitimu na kubobea katika Uislamu walijulikana kama ulamaa (maulamaa). Hali hii haikuzusha makundi ya Waislamu tu bali makundi ya wasomi na wafasiri wa dhana za dini ya Kiislamu miongoni mwa Waswahili. Ni maulamaa hawa ambao baadhi yao waliibuka kama watunzi wa tenzi za Kiswahili zilizosheheni maudhui ya dini ya Kiislamu. Sababu ya kusheheni maudhui hayo ya kidini ni:

a) Tafsiri za Kasida kutoka Uarabuni ambazo zilitumiwa kufafanua dhana za dini ya Kiislamu, zilichukuliwa na watunzi Waswahili kama tenzi na kuenziwa na Waswahili wote hasa kwa sababu ya kubeba maudhui yanayowalenga kimaisha.

b) Watunzi, kama vile Sayyid Nassir, walikuwa maulamaa waliohitimu mifumo ya dini ya Kiislamu katika madrasa.

c) Uislamu ulipoanza kukithiri miongoni mwa Waswahili uliathiri utamaduni na taratibu za maisha ya Waswahili. Hivyo basi Uislamu ulichukuliwa na Waswahili kama mwongozo kamili wa taratibu za maisha yao. Kama tujuavyo, fasihi zikiwemo pia tenzi, humulika utaratibu halisi wa maisha ya jamii. Kwa hiyo tenzi zilizotungwa hazikuepuka umulikaji wa maisha ya Mswahili ambayo yaliathiriwa na dini ya Kiislamu kama tunavyosoma katika tenzi za *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi*.

## 5.0 'Iktibasi' katika *Utenzi wa Mwanakupona*

*Utenzi wa Mwanakupona* ulitungwa na mwanamke, Mwanakupona Binti Mshamu Nabhanny, ambaye alizaliwa Pate mwaka 1810 (Mulokozi, 1999). Mtunzi anamlenga bintiye, Mwana Hashima bint Shee Mataka (1841-1933) ambaye wakati huo alikuwa amevunja ungo na karibu ataolewa.

Katika utenzi huu Mwanakupona anadhihirisha athari za Uislamu kwani anatumia dhahiri shahiri misingi ya dini ya Kiislamu inayohusiana na ndoa kutoka Kurani Tukufu na Sunnah kama tutakavyoona katika makala haya. Kwa mfano, athari za Uislamu katika *Utenzi wa Mwanakupona* zinatokana na nguzo ya kwanza ya Uislamu inayosema utangulize jina la Mwenyezi Mungu (S.W.T)

katika jambo lolote lile unalotaka kulifanya. Tunamwona Mwanakupona akifanya hivyo katika ubeti wa 4 hapo chini.

Pia kuna athari za matumizi ya msamiati wa Kiarabu. Hali hii inatokana na uhalisia kuwa Kurani Tukufu imeandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Kiarabu, kwa hivyo ni lugha jadi ya dini ya Kiislamu. Aidha, majina 99 ya Mwenyezi Mungu (S.W.T) ni ya Kiarabu. Uhitaji wa kumtaja Mwenyezi Mungu (S.W.T) kwa majina yake hufanya vigumu kukiuka utumiaji wa lugha ya Kiarabu katika dini ya Kiislamu. Hali hii inaonekana katika *Utenzi wa Mwanakupona*, mathalani:

Ukisa kutaqarabu
Bismillah kutubu
Umsalie Habibu
Na sahabaze pamoya (ubeti 4)

Maneno kama vile taqarabu, Bismillah, Habibu na Sahabaze yana asili ya Kiarabu.

Kwa hakika Kurani na Sunnah ndivyo vitu vya msingi katika maisha ya Mwislamu. Athari ya mafundisho kutoka Kurani Tukufu na Sunnah zinaonekana sana katika *Utenzi wa Mwanakupona* hasa pale tunapomwona mtunzi akisema katika ubeti wa 12:

La kwanda kamata dini
Faradhi usiikhini
Na sunna ikimkini
Ni wajibu kuitia (ubeti 12)

Katika Kurani Tukufu Luqman alimpa mwanawe nasaha juu ya jinsi anavyotakiwa kuwaheshimu wazazi, kuishi na wengine na kuomba Mwenyezi Mungu (S.W.T) kama inavyooneshwa katika Surat Luqman aya 13-19. Binti Mshamu, ambaye anatarajiwa kuolewa, anahitaji mno wosia wa jinsi ya kuishi na mumewe kwa msingi wa dini ya Kiislamu. Kwa mujibu wa mafundisho ya Luqman, mtunzi alijiona ana wajibu wa kumuusia bintiye na akachagua kutumia utunzi wa utenzi.

Wasia anaopewa binti Mshamu na mamake, Mwanakupona, umeorodheshwa kutoka ubeti wa 12-14 ambapo anaambiwa: jambo la kwanza ni ashike dini – dini ya Kiislamu, faradhi ni wajibu, na Sunnah asiikhini. Jambo la pili, anaambiwa awe na adabu na ulimi wa thawabu na popote aendapo awe mtu mahabubu. Jambo la tatu, anaambiwa asishirikiane na mtu asoshika haki. Baada ya wasia huu, Mwanakupona anamfahamisha bintiye kwamba mwanamke duniani

anapaswa apate radhi tano ndipo apate raha duniani na akhera. Radhi ya kwanza ni ya Mwenyezi Mungu (S.W.T), ya pili ni ya Mtume Muhammad (S.A.W), ya tatu ni ya baba, ya nne ni ya mama, na tano ni ya mumewe. Hata hivyo, badala ya kujikita zaidi katika radhi za Mwenyezi Mungu (S.W.T) na mtume Muhammad (S.A.W), Mwanakupona anajikita zaidi katika radhi ya mume, ambayo ndiyo inayohusiana na ndoa. Kurani, katika Surat An- Nisa inasema: 'Oeni mnaowapenda, mpende aliyekuoa na uwe mwadilifu'. Kwa msingi huu wa Kurani Tukufu tunamwona Mwanakupona aliona ana jukumu la kumuusia bintiye, anasema:

> Mwanangu twaa waadhi
> Pamoya na yangu radhi
> Mungu atakuhifadhi
> Akuepue na baa (Ub. 7)

Kisha anamtaka bintiye achukue mfano halisi wa yeye Mwanakupona na mumewe ambaye walioana kwa miaka mingi na hakumwonesha ovu lolote wala naye hakupata ovu lolote kutoka kwake. Waliishi kwa furaha na vicheko. Wasia wa Mwanakupona kwa bintiye kuhusu maisha ya ndoa unatokana na mafundisho ya Kurani Tukufu na Sunnah. Mathalani, katika Kurani Tukufu bibi zake Mtume Muhammad (S.A.W) wanachukuliwa kama mfano wa kuigwa na wanawake hasa kuhusu jinsi wanavyotakikana kuwa watiifu kwa waume zao. Katika Surat Al-Ahzab aya 30-31, Kurani inasema:

> "Enyi wake wa mtume, yeyote atakayefanya kosa la aibu, adhabu yake itakuwa mara mbili, na hili ni jambo rahisi kwa Mwenyezi Mungu (S.W.T), lakini (mke) atakayekuwa mtiifu kwa Mungu na Mtume, zawadi yake itakuwa mara mbili."

Kwa upande wa uhusiano kati ya mume na mke, Mtume Muhammad (S.A.W) pia anachukuliwa kama mfano wa wanaume. Tunasoma katika *Hadith* kauli ya Mtume Muhammad (S.A.W) kwamba "M'bora wenu nyinyi, m'bora wenu nyinyi ni yule aliyebora kwa mke (li-ahli) wake. Na mimi ni m'bora wenu kwa li-ahli wangu' (Khayrukum, Khayrukum li-ahli waana khayrukum li-ahli). Na Surat Al-Talaq aya 5 inasema:

> "Endapo yeye (mume) atakutaliki (mke) Mwenyezi Mungu (S.W.T) atampatia (mume huyo) wake wazuri zaidi yako ambao watakuwa watiifu na wenye kumwamini Mwenyezi Mungu (S.W.T) na Mtume (S.A.W)."

Hatimaye Kurani inatoa mifano ya wanawake ambao hawakuwa watiifu kwa waume wao na adhabu waliyopata. Surat Al-Tahrim aya ya 10 Kurani inasema:

> "Mwenyezi Mungu (S.W.T) anatoa mfano wa bibi wa Nuhu na bibi wa Luti kwa wale wasioamini. Wanawake hawa waliolewa na watu wawili wacha Mungu, lakini hawakuwa watiifu kwa wanaume wao na wakaambiwa 'Nendeni jehanam'"

Katika Kurani Tukufu na Sunnah vilevile Mwenyezi Mungu (S.W.T) anatoa mifano ya wanawake waliowatii waume wao. Katika Surat Al-Tahrim aya ya 11 Kurani Tukufu inasema kwamba bibi wa Pharao alifanya mema na akaenda peponi.

Ni dhahiri shahiri kwamba Mwanakupona bint Mshamu alibuni utenzi wake wa wasia kwa bintiye kwa misingi na athari ya ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah, na kwa misingi ya maisha ya ndoa ya Mtume Muhammad (S.A.W) ambayo, kama ilivyo katika *Hadith*, yalichukuliwa kama mafundisho na mifano kwa wanawake, hasa kuhusu maisha yao ya ndoa. Kutokana na ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah kuhusu mke katika ndoa, inadhihirika kutoka 'iktibasi' hii ya Mwanakupona kuwa mambo yafuatayo ni ya kimsingi kwa mwanamke hasa anapoolewa, ndipo Mwanakupona aliyasisitiza mambo yafuatayo:

a) Mwanamke amchukulie mumewe kama mlinzi na mkimu wa maisha yake. Huu ni uhalisia ambao ulikithiri Uarabuni na hata Uswahilini ambapo mke hakujishughulisha na shughuli nyingi za upataji riziki. Kwa mfano, miongoni mwa Waswahili, uvuvi ndio uliokuwa njia kuu ya kupata riziki, na hutekelezwa na wanaume pekee. Hali hii ilimfanya mwanamke amtegemee mumewe kama mlinzi na mkimu wa familia. Imani hii ndiyo iliyompelekea Mwanakupona kumuusia bintiye awe mwajibikaji kwa mumewe kwa kumwonesha mapenzi ya hali ya juu kulingana na utamaduni wa Waswahili kwa kumkanda, kumpepea na kumbembeleza, ili asimuudhi hata siku moja.

b) Mke akitalikiwa ama akimtaliki mumewe, basi ajue ya kwamba Mwenyezi Mungu (S.W.T) humpa mume huyo mwanamke mzuri zaidi. Ufunuo huu unamfanya mwanamke ajihadhari na ndoa, kwani endapo patatokea talaka basi ni yeye mwanamke atakayeathirika wala si mume. Kwa msingi huu Mwanakupona alimtahadharisha bintiye dhidi ya kumkosea mumewe, akijua talaka itamuathiri maishani mwake.

c) Mke kumtii mumewe ni njia mojawapo ya kumtii Mwenyezi Mungu (S.W.T) na mtume wake Muhammad (S.A.W), kwani ni Mwenyezi Mungu (S.W.T) ambaye amemfadhilisha mume zaidi ya mke. Mwanakupona alisisitiza radhi ya mume, akijua kwamba ni njia mojawapo ya mke kuongezewa thawabu na Mwenyezi Mungu (S.W.T).

d) Kuweko kwa mifano ya jehanamu kwa wanawake ambao hawawatii waume zao, kama Bi. Nuhu na Bi. Luti na mifano ya wanawake watiifu kwa wanaume zao kama bibi wa Pharao ambaye alienda peponi, kulimfanya Mwanakupona kutumia ufunuo huu kumsisitizia bintiye haja ya kumtii mumewe. Akijua kuwa kutomtii mume ni moja ya makosa yanayoweza kumpunguzia thawabu na kumpeleka motoni siku ya kiyama. Msisitizo huo aliuwasilisha kifasihi kwa kutia chumvi hasa pale alipouhusisha utiifu wa bintiye na radhi ya mumewe – kwamba asipomtii mumewe hatakuwa radhi naye na akisema atiwe jehanamu, basi atatiwa jehanamu. Vilevile, kutokana na ufunuo wa bibi wa Pharaoh, Mwanakupona alitumia mfano wa yeye mwenyewe kama mke aliyekuwa mtiifu kwa mumewe na wakaishi miaka mingi bila kukinzana, ishara ya kuwa hakumkosea mumewe na kwamba akhera aliko yuko radhi naye, hivyo basi anatarajia naye akifa ataenda peponi kwa radhi ya mumewe.

Mwanakupona, kama Mwislamu mwenye elimu na ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah, anatumia fasihi (utenzi) yake kuhimiza umuhimu wa kufuata maadili ya Kiislamu kama yanavyokaririwa katika Kurani Tukufu na Sunnah, hasa yanayohusiana na ndoa. Huu ndio mfumo wa 'iktibasi'. Kwa hakika, wasia wa Mwanakupona kwa bintiye Mwana Hashima ni kielelezo kwa wasichana wote wa janibu ya Kiislamu na isiyokuwa ya Kiislamu kwani katika moja ya beti za mwisho mwisho anasema:

Someni mite ya nganu
Mutii waume zenu
Msipatwe na zitunu
Za akhera na dunia (ubeti 95)

*Utenzi wa Mwanakupona* kwa kweli umejikita katika nguzo za Uislamu na mtunzi hakuna shaka alichota wasia huu kutoka Kurani Tukufu na Sunnah. Katika Surat Al- Nisa aya ya 25 Kurani Tukufu inashauri kuwa mke (wa kumwoa) awe Mwisilamu. Katika sura hii hii aya ya 35 Kurani Tukufu inasema: 'wanaume ni wakimu na walinzi (wa wanawake) kwa sababu Mwenyezi Mungu (S.W.T) amewafaradhisha. Hivyo basi wanawake wema ni wale wenye kutii waume zao wanaowalinda na kuwakimu'. Aidha, katika Surat-Al Ahzab aya ya 33 Kurani Tukufu inazungumza juu ya bibi wa mtume Muhammad (S.A.W)

kama mfano na kusema kwamba wanawake wanapaswa wakae nyumbani mwao, wasitoke ovyo ovyo ila panapo dharura na haja ya kufanya hivyo. Huu ni ushahidi unaochangia pia kuwa *Utenzi wa Mwanakupona* uliathirika kimaudhui na dini ya Kiislamu na kwamba wasia wake hivyo basi umejikita, kwa kiasi kikubwa, katika ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah kwa mfumo wa 'iktibasi'.

Kwa kuhitimisha, *Utenzi wa Mwanakupona* ni chombo na kielelezo cha uendelezaji wa Uislamu, kifasihi na wasia wote umechotwa kutoka kitabu Kitakatifu cha Kurani na Sunnah bila kutamka ya kwamba utunzi ulitokana na Kurani Tukufu. Huu ndio mfano halisi wa mfumo wa 'iktibasi' katika Uislamu.

### 6.0 'Iktibasi' katika *Utenzi wa Al-Inkishafi*

Mtunzi wa utenzi huu ni Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir ambaye alikuwa mwenyeji wa Pate. Kulingana na makadirio ya Hichens (1972: 9) mtunzi aliishi baina ya miaka ya 1720 na 1820 ilhali Chiraghdin na Mnyampala (1969) wanasema mtunzi wa utenzi huu aliishi baina ya miaka ya 1718 na 1815. Mtunzi Sayyid Abdallah alitoka ukoo wa malenga na yeye mwenyewe alikuwa maulama, yaani mwenye kufuzu katika elimu ya dini ya Kiislamu. Kulingana na ujuzi wake wa dini na tajiriba yake kama mwalimu wa Kiislamu Sayyid Abdallah alibaini haja ya kutumia fasihi kama chombo cha kutoa mafundisho ya dini ya Kiislamu. Na kwa hakika utenzi huu umetungwa kwa misingi ya dini ya Kiislamu kwa mfumo wa 'iktibasi'. Aliutunga kwa minajili ya kuunasihi na kuuonya moyo wake utubie na kutenda mambo ya haki ili siku ya kiyama uende peponi.

Sayyid bin Abdallah alitunga utenzi kwa kuupanga katika daraja. Anaanza kwa shahada, yaani kutaja jina la Mwenyezi Mungu (S.W.T) kama ilivyo kawaida katika dini ya Kiislamu. Anaanza:

> Bismillahi naikadimu
> Hali ya kutunga hino nudhumu
> Na ar-Rahmani kiirasimu
> Basi ar-Rahimi nyuma ikaye (ubeti 1)

Anaendeleza shahada kutoka ubeti wa 1-5 na kumsalia ama kumtakia rehema Mtume Muhammad (S.A.W) na sahabaze wanne (R.A).

Ubeti wa 6 ni kivukio kutoka shahada hadi dhamira. Kutoka ubeti wa 7 Sayyid bin Abdallah anatoa dhamira yake ya kutunga utenzi huu. Mtunzi anajiona ni mwenye dhambi na dhamira yake ni kuunasihi moyo wake ambao umetekwa na hawaa za ulimwengu na shetani. Kwa hiyo, mtunzi anatumaini kwamba baada ya kuzungumza na moyo wake, moyo utayashika yote na kushawishika na kutenda

yaliyo ya haki mbele za Mwenyezi Mungu (S.W.T) kama Kurani Tukufu na Sunnah katika dini ya Kiislamu zinavyofundisha. Vilevile, mtunzi anasema kwamba utenzi huu unanuiwa kuwazindua pia wale wasomaji ambao wamo katika dau moja na moyo wake, kwa kuwapa mifano ya dunia ilivyo kwa kutumia jazanda za ulimwengu, kama vile kuinasibisha dunia na bahari tesi, kisima kisicho kina, vumbi la mwangaza na meto. Baada ya mifano hiyo mtunzi anaunasihi tena moyo wake utubie. Anasema:

> Kimakwe kuisa dibaji yangu
> Penda kuuonya na moyo wangu
> Utetwe ni hawa ya ulimwengu
> Hila za Rajimi ziughuriye (ubeti 10)

Katika daraja la nne, mtunzi anaupa moyo wake mifano ya maisha ya watu wa Pate yalivyokuwa, na kwamba maisha si chochote wala si lolote kwani wote hawa walikufa. Baada ya daraja hili mtunzi anauliza moyo wake kama umeshawishika. Lakini anahisi bado, kwani katika daraja la tano, anaupa moyo wake mifano ya wazazi wake na viongozi wa Pate Yunga, na baadaye anaupa moyo wake pia mifano ya mitume. Anasema:

> Hakuwa mtumi Suleimani
> Maliki wa insi na ajinani
> Ulimfutuye ukamukhini
> Akiwa mwengine, wamtendaye? (ubeti 32)
>
> Uwapi Ali bin Nassir,
> Na muwamu wake Abubakari,
> Mwinyi Idarusi na Muhadhari?
> Wendelepi kuwe mbonya ndiaye? (ubeti 57)
>
> Moyo ya kwamba ya watu sao
> Kalamu ya Mungu iwapeteo
> Nawe wa yakini kuwa kamao
> Au una yako uyashishiye? (ubeti 64)

Mtunzi anaukumbusha moyo wake kwamba hawa wote, mitume na shemeji zake, wamekufa. Hivyo basi, moyo wake pia hautaepuka kifo. Swali ni: "Baada ya kifo, moyo wake utaenda wapi? Peponi ama jehanamu?

Katika daraja la sita, mtunzi anaufunulia moyo wake hali itakavyokuwa jehanamu ambako utakwenda ikiwa hautatubia. Anataja baadhi ya myoto, kama

vile moto wa Hawiya, moto wa Sairi, moto wa Ladha na moto wa Hutama kama myoto ya adhabu inayoungojea moyo wake jehanamu ukiwa hautatubu. Mtunzi anasema:

> Kuna na Hawiya, pulika sana
> Ni moto mkali, hau makina
> Asi aingiapo hula kitama
> Huona pumzi zimsiziye (ubeti 74)

Baada ya kuufunulia moyo wake kila aina ya moto na adhabu zake, mshairi anausihi moyo wake mara ya mwisho ili utubie. Ni matumaini yetu kuwa moyo wa mshairi ulitubia ili na sisi utenzi huu uwe toba kwetu. Kwa hakika, katika *Utenzi wa Al-Inkishafi*, Nassir ametumia Kurani Tukufu na Sunnah kama msingi wa utenzi wake bila yeye kutuambia hivyo. Hii ndiyo hali inayorejelewa kama 'iktibasi'. Kwa mfano, katika Surat Ash-Shura aya ya 7, Kurani inasema:

> "Tumemfunulia Kurani kwa Kiarabu ili muweze kuwaonya watu wa miji na wale wote wanaoishi katika viunga vyao, kuhusu siku ya kiyama ambapo wengine wataenda peponi na wengine jehanamu."

Ufunuo huu ndio uliomfanya Nassir kujihisi kuwa ana wajibu wa kuwahubiria watu, hasa wale ambao wanatenda dhambi. Nassir alichagua kutumia mbinu ya 'iktibasi' ya fasihi ya uzungumzi nafsia kwa kuzungumza na moyo wake kama kielelezo cha nyoyo za watu wengi wengine wenye dhambi.

Kulingana na Kurani Tukufu na Sunnah (Surat Al-Imran aya ya 185) kila roho itakufa. Lakini swali kuu ni: Baada ya kufa roho yako itaenda wapi? Kurani Tukufu na Sunnah inasema kuna siku ya kiyama ambayo aijuaye ni Mwenyezi Mungu (S.W.T) pekee, na siku hiyo kila mmoja atafunguliwa shajara ya matendo yake hapa duniani. Ikiwa mtu alitenda maovu basi ataenda motoni (Surat Ibrahim aya ya 29). Katika Surat Al-Humazah aya ya 4, Hutama unatajwa kama mfano wa myoto iliyoko jehanamu. Endapo mtu atakuwa ametenda mema, basi ataenda peponi na kuishi kwenye bustani ya Eden yenye vijito vinavyobubujika maji milele kama tunavyofunuliwa katika Kurani Tukufu na Sunnah (Surat Al-Imran aya ya 136) kama alivyoahidi Mwenyezi Mungu (S.W.T). Kurani Tukufu inasema:

> "Mwenyezi Mungu (S.W.T) ni mwingi wa rehema, na atakayebadilisha kutenda maovu na atende mema na ya haki, basi yeye atasamehewa (Surat An-Nisa aya ya 110, Surat Al-Taubah aya ya 112 na Surat Al-Furqan aya ya 70)".

Kurani Tukufu na Sunnah, kama mwongozo kamili wa maisha ya wanadamu (Surat Bani Isra-il aya ya 105, Surat Ta-Ha aya ya 113, Surat An-Nami aya ya 1-3 na Surat Luqman aya ya 3) inasisitiza ya kwamba watu wote wanaoamini, wajitayarishe, watubu ili wasiende motoni. Kutubu kama njia pekee ya kwenda peponi pia inasisitizwa katika Surat Al-Haji aya ya 49 hasa huhusu adhabu ya dhambi ambayo ni machungu na mateso yatakayotokana na moto wa milele (Surat Al-Taubah aya ya 3 ana Surat Al-Inshiqaq aya ya 24).

Katika Kurani Tukufu na Sunnah tunaelezwa waziwazi kuwa wale wasioamini wamepatwa na hawaa ya maisha ya ulimwengu na kudanganyika kwa kuona maisha ya dunia hii ni mazuri kuliko maisha ya peponi (Surat Al-Taubah aya ya 38, Surat An-Najim aya ya 29 na Surat Al-A'la aya ya 16-17). Ili kuwaonya watu kama hawa ambao hawaamini, Kurani Tukufu na Sunnah inatumia maonyo dhidi ya adhabu ya dhambi (Surat Al-An-Am aya ya15 na Surat Az-Zumar aya 16) ambayo ni moto na pia kumwonesha mwanadamu kuwa yeye na maisha yake ya duniani si lolote wala chochote mbele ya Mwenyezi Mungu (S.W.T) kama inavyodhihirika katika Kurani Tukufu katika Surat Al-Imran aya ya 185, Surat An-Nisa aya ya 94 na Surat Hud aya ya 15. Kurani Tukufu na Sunnah vilevile inamfunulia mwanadamu ishara na mifano kadha wa kadha, hasa ya miji mingi ilivyoharibiwa na Mwenyezi Mungu (S.W.T) na kuanguka kama inavyodhihirika katika sura zifuatazo za Kurani Tukufu na Sunnah (Surat Al-Imran aya ya 137, Surat Muhammad aya ya 10 na Surat An-Anam aya ya 104). Mifano zaidi inapatikana katika sura za Al-Haqqah aya ya 3-4 ambapo jamii ya Thamud iliangamizwa kwa janga la mafuriko.

Vilevile, Kurani Tukufu na Sunnah inatumia mifano ya vizazi vingine vingi vilivyopita na kuangamizwa na Mwenyezi Mungu (S.W.T) kwa maafa mbalimbali, na kwamba vizazi vyote vimepita na havirudi tena (Surat Al-Taubah aya ya 70). Mifano hii ni ishara zaidi kwa mwanadamu kuwa yeye na maisha yake si chochote wala lolote mbele ya Mwenyezi Mungu (S.W.T.). Ujumbe ni kwamba lazima roho zote zitakufa. Swali ni: Baada ya kifo roho yako msomaji, kama ile ya Nassir, unataka iende wapi?

Kulingana na ufunuo huu ambao tumeutanguliza, ni dhahiri shahiri kuwa Nassir alichota taarifa yake kutoka Kurani Tukufu na Sunnah na kwa ufundi wa kifasihi akaihalisisha taarifa hiyo kwa kutumia mfumo wa 'iktibasi' wa maonyo kwa moyo wake na mifano ya vifo vya jamii yake na kuanguka kwa mji wa Pate kama ishara ya kwamba, kwa vyovyote vile roho itakufa kama jamii za Nassir walivyokufa na Pate kuangamia na kuanguka. Swali kuu tena ni: Baada ya kifo roho itaenda wapi?

Kwa kiasi kikubwa mtunzi wa *Al-Inkshafi* aliathiriwa na dini ya Kiislamu, kwanza kutokana na ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah kuwa yeye ana wajibu wa kuwaonya watu wasioamini Mwenyezi Mungu (S.W.T). Wajibu huo ameutekeleza kifasihi ambapo ametumia mbinu ya 'iktibasi' kuuonya moyo wake kwa uzungumzi nafsia, kama kielelezo cha nafsi za watu wasiomwamini Mwenyezi Mungu (S.W.T). Anauonya moyo wake na kuuonesha kuwa maisha duniani si kitu. Anaendelea kuuogofya moyo wake kwa adhabu za kifo ambazo ni machungu ya myoto. Anaupatia mifano ya wazazi wake na wengine kuwa wao pia walikufa na kwamba nao mioyo yao haitaepuka kifo. Yote haya mtunzi anayaeleza kwa misingi ya ufunuo wa Kurani Tukufu na Sunnah. Ndipo mwisho anausihi moyo wake unabihike kwani hapendi moyo wake uende jehanamu bali peponi.

Kwa kuathiriwa sana na Kurani Tukufu na Sunnah Nassir anauona Uislamu kama njia ya kumwokoa mwenye dhambi ambaye anahadaiwa na maisha ya ulimwengu. Mtunzi ametumia mafundisho ya Kurani Tukufu na Sunnah na kuwapa wasomaji Waswahili mfano halisi wa mji wa Pate ambao wanaujua na vizazi wavijuavyo ili kuleta mahubiri yake karibu zaidi na jamii ya Waswahili waliokusudiwa utenzi huu nyakati hizo ili wapate kuuelewa zaidi badala ya kutumia mifano inayotolewa katika Kurani Tukufu na Sunnah.

Mtunzi anajipa matumaini, na sisi wasomaji pia, kwamba nyoyo zikitubu basi hazitaenda jehanamu kwenye moto, bali zitaenda peponi. Surat Al-Nisa aya ya 110 katika Kurani inasema:

> "Mwenye kutenda maovu kisha akaomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu (S.W.T) atamkuta Mwenyezi Mungu (S.W.T) ni mwenye kughufiria na kurehemu."

**7.0 Hitimisho**

Katika tenzi zote mbili, *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi* imedhihirika kwamba tenzi za kale zilitumika kama chombo cha kuhubiria dini ya Kiislamu kwa kupitia mfumo wa 'iktibasi' ambapo watunzi walichota mafundisho kutoka Kurani Tukufu na Sunnah na kutumia fasihi kama ngazi ya kufundishia mafundisho hayo kwa Waswahili. Hii inadhihirisha kwamba fasihi kama kioo cha jamii inaweza kutumika sana kueneza mafundisho na maadili ya Kiislamu hasa kwa wananchi wa kawaida ambao pengine hawajui kusoma Kurani Tukufu kwa Kiarabu. Ni matumaini ya watunzi wote wawili kwamba tungo zao zilisomwa na Waislamu na wasiokuwa Waislamu na wakahubirika na mpaka sasa yeyote atakayesoma tenzi hizi ataendelea kuhubirika na kuacha maovu na kufuata yaliyo ya haki kwa

misingi ya dini ya Kiislamu. Hali hii inafanya tuchukue tenzi za kale za Kiswahili kuwa zina jukumu muhimu kama chombo cha kuhubiria mafundisho ya Uislamu kifasihi kupitia mfumo wa 'iktibasi'. Hapo zamani tenzi zilitumiwa sana kuelezea mafundisho ya dini ya Kiislamu mpaka kufikia wakati iliposemekana ushairi wa Kiswahili umetolewa uwanjani na kupelekwa msikitini. Hivi sasa utunzi wa tenzi si mwingi kama ulivyokuwa nyakati za kina Mwanakupona na Sayyid Nassir. Hivi sasa mashairi ndiyo yanayotungwa zaidi kuliko tenzi. Ni hivi karibuni tu tumeona Ahmed Sheikh Nabhanny (1971) akitunga *Utenzi wa Mwangaza wa Dini* akielezea wajibu wa Mwislamu kwa Mwenyezi Mungu (S.W.T). Kuna haja ya kufanya mikakati ya kurudisha mashairi na tenzi misikitini ili watu wanapoburudishwa na mashairi na tenzi hizo waburudishwe pamoja na kupata mafundisho ya dini ya Uislamu.

## Marejeo


Ahmed, A. (1986). *Al-Quron: A Contemporary Translation*, Karachi: Akrash Publishings.

Roded, R. (1999). *Women in Islam and the Middle East: A Reader*. London: I.B. Tauris Publishers.

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar-es-salaam: TUKI.

Shahid, I. (1980). "Arabic Literature" in Holt (1991) *Cambridge History of Islam*. Vol. 2B Cambridge University Press Pg. 657-671.

Shihabdhin, S. & Munyampala, M. (1974) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Abdulaziz, M.H. (1994). *Muyaka: 19$^{th}$ Century Swahili Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Al-Farsy, S.S. (1991). *Kurani Tukufu* (Tafsiri). Nairobi: Nairobi Islamic Foundation.

Allen, J.W. (1977). *Al – Inkishafi : Catechisim of the Soul*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Hichens, W. (1972), *Al - Inkishafi:The Soul's Awakening*. London: Oxford Univfrsity Press.

Nabhanny A.S. & Abubakar, A.S. (1992) *Utenzi wa Mwanakupona*. Nairobi: Heinnman.

Yar – Shater, E. (1980). "Arabic Literature'' in Holt (1991). *Cambridge History of Islam*. Vol 2B, Cambridge: Cambridge University. Press Pg. 672 - 681.

Ibrahim N. S. (1991). "Islam and Secularity in Swahili Literature: An Overview" in Harrow, W. K (edt) *Faces of Islam in African Literature* pp 37 – 58.

Biersteker, A (1991). "Language Poetry and Power: A Reconstruction of Utendi wa Mwanakupona" in Harrow (edt) *Faces of Islam in African Literature* pp 37 – 58.

Mulokozi, M. M.& Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nabhanny, A. S. (1971). *Utenzi wa Mwangaza wa Dini*. Mombasa: Coronation Printers.

Taib, A. H. (2004). 'Mafundisho ya Uislamu katika kazi za Shaaban Bin Robert'. Tasnifu ya MA Kiswahili. Islamic University in Uganda. Haijachapishwa.

Maulana, M. A. (1986). *The Religion of Islam: A Comprehensive Discussion of the Sourses, Principles and Practices of Islam*. Delhi: Taj Company.